



Imeletwa kwenu na:

YITA youth initiatives tanzania

ikishirikiana na:



Taarifa kwa Vyombo vya Habari  
Kwa usambazaji wa haraka

## Bei ya dawa za kutibu malaria yabainika kuzidi ile iliyopendekezwa na Serikali Licha ya mpango wa ruzuku, utafiti jijini Dar es Salaam unaonyesha wananchi wanalipishwa zaidi

**9 Oktoba 2013:** Maduka kadhaa ya dawa jijini Dar es Salaam yanaendelea kuuza dawa ya kutibu malaria kwa bei isiyohi kwa dozi za watoto na watu wazima.

Matokeo haya yalitolewa katika muhtasari ulioendeshwa na Shirika la Vijana la Kujitolea Tanzania (*Youth Initiatives Tanzania*, YITA) uitwao: *Gharama ya kutibu malaria: Je, Serikali, wahisani, sekta binafsi na wananchi wanaweza kuhakikisha dawa za gharama nafuu?* Matokeo hayo yanatokana na utafiti uliofanyika katika maduka ya dawa 58 yaliyopo katika wilaya zote tatu za jiji la Dar es Salaam. Wafanyakazi wa YITA walitembelea maduka haya na kununua dawa ya Artemether-lumefantrine (Alu), ambayo ni dawa inayopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kutibu malaria.

Dawa ya Alu ilichaguliwa kufuatia mpango wa majaribio wa Dawa Nafuu za Malaria (AMFm). Mpango huu uliofadhiliwa na Mfuko wa Ulimwengu wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria ulianzishwa ukiwa pia na nia ya kuwezesha uagizaji bidhaa katika sekta binafsi na za umma kufanikiwa kununua dawa ya Alu yenye ruzuku. Tanzania ni miongoni mwa nchi saba za Afrika zilizoshirikishwa katika majaribio ya AMFm na kutoa matokeo ya kuwa bei ya dozi ya mtu mzima iwe TZS 1,000 na ile ya mtoto iwe TZS 500. Bei hii imehimizwa kupitia vituo vya televisheni na redio na hata matangazo yanayobandikwa hasa katika maeneo ya umma. Matangazo haya yalitolewa kupitia taarifa za ofisi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuanzia Julai na Agosti 2011. Mabango na vipeperushi pia vilitumika kuhamasisha jamii vikionyesha bei ya Alu inayoelekezwa na Serikali.

Utafiti uliibua mambo yafuatayo:

- Kati ya maduka ya dawa 55 yaliyouza dozi ya mtoto ya Alu, karibu yote yalidai TZS 1,000 au zaidi. Ni duka moja tu ndilo lililokuwa likiua dawa hiyo kwa bei sahihi ya TZS 500 kwa dozi hiyo ya mtoto.
- Kwa upande wa dozi ya watu wazima, ilibainika kuwa duka moja kati ya mawili (48%) yaliuza Alu kwa bei zaidi ya TZS 1,000. Karibu robo (23%) ziliuza Alu kwa TZS 2,000 au zaidi.
- Vilevile, kulikuwa na tofauti katika wilaya moja hadi nyingine – wilaya tajiri zilikuwa uwezo mkubwa zaidi wa kuuza Alu kwa bei kubwa zaidi. Karibu nusu ya maduka ya dawa Kinondoni (47%) yaliuza Alu kwa TZS 2,000 au zaidi wakati katika wilaya ya Temeke, zaidi ya robo tatu (79%) ya maduka ya dawa yaliuza Alu kwa bei iliyopendekezwa ya TZS 1,000.

Programu ya ruzuku imefaulu kwa kiwango fulani: Bila mpango huu, dawa ya Alu ingezwa kwa Dola kati ya 10 na 15 au kati ya TZS 16,000 na 24,000 (bei isiyohi na ruzuku). Hata hivyo, licha ya jitihada za Serikali, wahisani na sekta binafsi, bado dawa hii inauzwa kwa bei ya juu zaidi kuliko ile iliyowekwa na Serikali.

Abner Okello, Mkurugenzi Mtendaji wa YITA alisema *“Pengo lililopo kati ya bei iliyopendekezwa na bei halisi ni tishio kwa jitihada za kukabiliana na malaria na halina budi kushughulikiwa. Mamlaka ya Chakula na Dawa ina jukumu la kusimamia bei ya dawa lakini huenda inakabiliana na changamoto katika kudhibiti bei nchini kote. Pengine wanaweza kubuni njia ya kutumia ujumbe mfupi wa maneno kwa njia ya simu ambayo ingeweza wananchi kutoa taarifa iwapo bei waliyonunulia Alu ipo upande wa juu. Hili lingengeza nguvu kwenye jitihada zilizopo sasa.”*

--- Mwisho ---

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na :**

**Tunu Yongolo**

**Afisa Mawasiliano, Twaweza**

**baruapepe:** tyongolo@twaweza.org | **simu:** +255 752 833 860

**Maelezo kwa Wahariri**

- Youth Initiatives Tanzania (YITA) husaidia makundi ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 30 katika eneo la Manzese. Kwa msada wa YITA, vikundi hivyo vinalenga kuwasaidia kuanzisha shughuli endelevu za kuingiza kipato. Taasisi inaendesha program ya mafunzo ya miaka mitatu katika ujasiriamali na hutoa msaada wa vifaa.
- Unaweza kufuatilia kazi ya YITA: [yitanzania.wordpress.com](http://yitanzania.wordpress.com)
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayoamsha msukumo wa kiraia na ambayo inalenga kuleta mabadiliko makubwa katika Afrika ya Mashariki. Twaweza inaamini kwamba mabadiliko ya kudumu huhitaji msukumo unaoanzia chini, na inatafuta kukuza hali na kupanua fursa ambazo kwazo mamilioni ya watu wanaweza kupata taarifa na kufanya mabadiliko hayo yatokee katika jamii zao na hasa kwa kuziwajibisha serikali moja kwa moja.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:

**Tovuti:** [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org) **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza\_NiSisi